

KITUMBUA CHA MAUTI

NA HADITHI NYINGINE

Wahariri

Kaka FRED

John Ustadh KAMAU

Okwalo WAMBANI

KITUMBUA CHA MAUTI
Na Hadithi Nyingine.

Imechapishwa kwa mara ya kwanza 2022.

Haki zote zimehifadhiwa. Ni marufuku na hatia kwa wenye silika za kugushi, kuiga, kubadili, kuchapisha, kutafsiri, kuigiza au kutumia mbinu zozote bila idhini ya wandishi kupitia kwa wakili wao.

Mtu yeyote atakayefanya kitendo chochote kinyume cha sheria ataweza kushtakiwa.

ISBN : 979-8805-93-797-3

Wahariri

Kaka Fred: +254716349065

Baruapepe: kakafred25@gmail.com

Okwalo Wambani: +254718885767

John Ustadh Kamau: +254711879421

Baruapepe: ustadhkamauelimu@gmail.com

YALIYOMO

YALIYOMO	iii
DIBAJI	iv
KITENDAWILI CHA MAISHA na Mwalimu Sammy	5
KITUMBUA CHA MAUTI na Okwalo Wambani ..Error! Bookmark not defined.	
CHAO NI CHANGU na Kaka Fred Error! Bookmark not defined.	
BAADA YA UHURU na John ‘Ustadh’ KamauError! Bookmark not defined.	
MAGUGU na Humphrey Onkoba Error! Bookmark not defined.	
MKONO WA JASUSI na Bi. Esther Wachira .Error! Bookmark not defined.	
ADHABU YA KIVUMBI na Elizabeth Barasa Error! Bookmark not defined.	
CHOZI LA SAMAKI na Bonface Ambunya Error! Bookmark not defined.	
SIRI YA MAUTI na Anusu Joshua Error! Bookmark not defined.	
NIZIKENI NIFAPO na Eliud Mukungu ‘The Great’ Error! Bookmark not defined.	
HATIMA YA YATIMA na Loreen Amugune ... Error! Bookmark not defined.	
MIALE YA MATUMAINI na D.N Matheri Error! Bookmark not defined.	
CHOZI LA MASIKA na Lindah Kagoitsi Error! Bookmark not defined.	

NDOTO YA SHARI na *Wanjohi P. Mugambi..* Error! Bookmark not defined.

SAFARI YA KESHO na *Ndombi C. Wawire...* Error! Bookmark not defined.

MCHIMBA KISIMA na *Shariff Ommito.....* Error! Bookmark not defined.

SHEREHE Error! Bookmark not defined.

DIBAJI

Katika pilkapilka za kulivuka daraja la ukata ili kuupakata ukwasi, wapo watumiao njia mkato na wapo wajitumao kwa bidii na haki wakimaizi kuwa hawafai kuwa kupe. Kitumbua cha Mauti ni antholojia iliyosukwa ikasukika kama mswala.

Imejumuisha waandishi wenye utaalamu wa hali ya juu na wenye macho mapevu yaliyoangaza maudhui ya kisasa. Inajivunia anwani anuai zenye mafunzo ya hekima na tabasuri zinazotahadharisha na kueneza injili ya usawa na kupinga mitazamo hasi katika jamii ya wanaleo.

Wahariri wamepiga mbizi na kuzuka na upanzi muafaka utakaokufanya ukienzi Kiswahili na fasihi. *Kaka Fred, Ustadh Kamau* na *Okwalo Wambani* ni mfano tosha wa wahariri mahiri wa fasihi.

Visa vina tamathali aali aali zitakazomfanya msomi kutoiweka chini nakala hii. Ama kweli hutahema na kushika tama kwa

kujinyakulia diwani hii. Usingoje kuhadithiwa jamani. Kaa mkao wa kula.

Kaka Fred
na
Ustadh Kamau

KITENDAWILI CHA MAISHA na Mwalimu Sammy

Sammy Oluoch almaarufu *Mwalimu Sammy* ni mwalimu mshtiti wa lugha ya Kiswahili katika shule ya *Utawala* kaunti ya Narok. Amekuwa mstari wa kilele kuhanikiza lugha ya Kiswahili kupitia kwenye vyombo vya habari. Ameandika: *Siri za Insha Aula, Kisima cha Mkata, Mwamba wa dhahabu na Hadithi Nyingine* pamoja na *Zawadi ya baba na Hadithi Nyingine*

Hatimaye mwangaza angavu wa jua ulisalimu amri. Uliyeyuka na kutokomea kama barafu motoni. Giza totoro la maki likabisha na kushika usukani. Saa moja, saa mbili, saa tatu, saa nne. Usiku uliyasukuma majira kwa kasi ya duma. Usiku wa mashetani ukasogea na kujongea namna fisi mlafi anayebanwa na ubao anavyoandama harufu ya mzoga. Usiku ulikuwa mtulivu bila rabsha wala kelele zozote. Kila mwili wa viumbe ulitii amri ya usingizi. Kunao waja waliozama kwenye gonezi la pono na wengine la mang'amung'amu. Mbwa, fisi, kereng'ende na viumbe wote walikuwa wafu usiku huo. Mwanguko wa sarafu hakika ungesikika kama mlipuko wa bomu la wanajeshi wa Urusi kule katika taifa la Ukreni.

Kitandani nilijifunika gubigubi na kutulia tuli kama maji ya kuzi. Sikuambulia hata lepe la usingizi. Usingizi ulinikataa. Macho yakadinda kufumbika. Aliyeniona akiwemo dada yangu mlunguzi angetuhumu kuwa nilikuwa nimezama zi kwenye gonezi la pono. Lakini wapi? Nilikuwa macho kama mbwa wa kachero aliye tayari kwa taharuki yoyote. Kisa na maana, dada yangu mlunguzi tuliyelala naye kwenye kitanda chetu cha mayowe hakuwa amezilaza na kuzinyosha mbavu zake samadarini hata kwa sekunde moja. Saa nane za usiku alikuwa macho. Akili zilimzungusha duniani. Alivyozi kuwaza na kuwazua ndivyo nami nilivyozi kutafakari na kutafakuri kuhusu lililomsibu usiku huo wa manane.

Mama alitembelewa na mgeni ghafla alipokuwa hospitalini. Alikuwa amehimili. Kwa mara ya pili katika maisha yake. Alikuwa hospitalini akikabiliana na uchungu wa uzazi. Papo hapo mgeni akajitoma chumbani mle mwa uzazi. Wengi hawakumtambua ila tabibu mkuu aliyekuwa akimhudumia mama. Daktari alionekana kujawa na hawafu nyingi. Hakuna aliyefahamu hasa kiini cha wasiwasi ule. Kumbe alimfahamu fika yule mgeni. Haikuwa mara ya kwanza kukumbana naye katika huduma

zake pale hospitalini. Hata hivyo, mara hii hakutaka kumkaribisha. Lakini wapi? Mwenye nguvu mpishe. Mgeni yule alikuwa Izraili! Ni nani angemkaribisha kwa furaha riboribo? Izraili alimpokea mama naye mnuna wangu akajipata duniani kwa upasuaji.

Tangu mama alipokumbatiwa na Izraili mawazo chungu nzima yamekuwa yakituteka bomani mle. Mimi bahati sikuwa mwana halali wa baba yangu. Mama aliolewa akiwa pamoja nami. Pindi mama alipofarakana na sayari ya tatu baba hakukawia kupata jiko tena. Alimwoa Katili, mwanamke aliyekuwa na urembo unaozidi wa tausi. Licha ya mama wa kambo kutudharau na kutufanyisha kazi za sulubu baba alitufariji kwa mapenzi ya mzazi. Alijipinda mgongo na kujifunga kibwebwe kuhakikisha kuwa tumepata elimu. Shuleni kamwe hatukuwa visu butu. Tulijikaza kisabuni tukitumai kuwa ipo siku tungeyakidhi mahitaji ya familia yetu na jamii yetu iliyozama kwenye tamaduni za jadi.

Ni tamaduni hizi ndizo zilizomkaribisha izraili mle hospitalini. Licha ya mama kuupinga ukeketaji wa wasichana kwa jino na ukucha wazazi wa mama yangu hawakusikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Waliafikiana kumtafutia mchumba akiwa katika gredi ya sita. Alikuwa binti mdogo sana. Darasani mwao ndiye aliyekuwa mdogo zaidi. Wengine walishuku kuwa huenda hakupitia gredi zote. Hata hivyo, werevu wake na ufahamu mpana aliokuwa nao uliwashawishi wote kuwa aliizidi gredi ile ya sita. Mchumba aliyetafutiwa - baba yangu – alikuwa tajiri wa kutajika. Aliyamiliki yote ambayo mja angeyatamani duniani. Utajiri huu ndio uliokuwa msukumo mkubwa zaidi kwa wazazi wake kumwoza. Alikuwa chambo cha kunasa utajiri. Alionekana kutosha kuwavusha kutoka katika bahari ya uchochole hadi kwenye kisiwa cha ubwanyenye. Kichwa chake chepesi na ndoto yake ya kuwa daktari zote zikazikwa katika kaburi la saha.

Majukumu yote yalimkaba. Si ya jikoni, si ya sebuleni, si ya shambani, si ya kitini si ya kitandani. Kulingana na mila yao katu asingerudi kwao. Iwapo angerudi angeipata ikiwa jehanamu. Ulikuwa mwiko kwa aliyeoleka kurejea nyumbani kwa sababu ya kukosa amani katika boma lake. Mama alihimili. Ukeketaji ule ulimnyima kupata salama. Akajifungua kwa operesheni. Nikaliona jua kwa mara ya kwanza. Nikaujua umuhimu wa hewa safi. Pengine hii ndiyo maana katika harakati zangu zote nilihubiri injili ya upanzi wa miti na utunzaji wa mazingira.

Katika boma lile hakukuwa na mwanamke hata mmoja aliyewahi kujifungua akapata mvulana. Hali hii ilizidisha machungu ya mama. Hata akatelekezwa baada ya mimba ya pili. Alipelekwa hospitalini nao utafiti wa matabibu ukabaini waziwazi kuwa malaika tumboni alikuwa wa kike.

Madharau dhidi ya baba kijijini hayakumpa amani. Mahirimu wake mara nyingi walimwita ‘asiye na mrithi.’ Baada ya kujawa na hasira za mkizi alihamia mjini. Aliwaacha wale ‘mabaradhuli,’ kama alivyowaita wake, nyumbani. Kule mjini anasa ilimnasa. Hakujinasua. Akasalimu amri mkononi mwa ugonjwa wa ukimwi miongoni mwa ndwele nyingine za zinaa. Ami zetu walimdhulumu mama sana. Kunao waliojitolea mhanga kumrithi ili awe mke wao. Kunao waliodai kuwa hakuwa na haki ya kumiliki chochote isipokuwa hewa ya kupumua. Adui wa mwanamke ni mwanamke mwenzake. Wakewenza waliungana kuzidisha uchungu wa mama. Walizichukua zote walizoon. Baada ya mama kuachiwa nguo zilizokuwa mwilini pake, sakafu ya nyumba yake na hewa ya kupumua alionyeshwa njia. Kabla ya mama kuondoka uchungu wa uzazi ukamnyima ruhusa ya kuondoka kwa haraka namna aliyoomriwa na wakewenza.

Mama alijipata hospitalini. Ni hospitalini huko ndiko alikopokelewa na Izraili. Tulilelewa nyumbani kule kwa miaka kadhaa toka utotoni mwetu. Hatimaye zamu yetu ya kuondoka iliwadia. Tulifurushwa kutoka nyumbani mle. ‘Mama’ zetu walitulilia ngoa kutokana na ufanisi mkubwa tuliokuwa nao shuleni. Wana wao walikuwa mbumbumbu wasioweza kuunga moja na moja wakapate mbili. Walitugeza kuwa vitega uchumi kwao. Tuliuzi maji na ndizi mitaani bila kuonja wala kunywa. Hata kiu ilipotusakama tulikufa kikondoo. Kilichotokea Jumamosi moja ingali mawazoni. Ilikuwa siku ya soko kijijini. Nilibeba ndizi nzito kama nanga naye mnuna wangu alibeba maji chupa kadhaa. Tulipofika na kuwasili sokoni, tulikumbana ana kwa ana na chifu. Alikataa katakata kuturuhusu kuingia sokoni. Alisisitiza kwamba tulikuwa wachanga kushiriki biashara ile.

Tulimrai na kumbembeleza aturuhusu waama tungethubutu kurudi jehanamuni bila hela tungeburudishwa na kilichomtoa kanga manyoya. Hatukukata tamaa kumwomba ruhusa. Alipoona kuwa hatukuwa tukilegeza kamba kuhusiana na msimamo wetu, aliwasilisha wazo lake. “Ili niwaruhusu kuingia humu ni lazima kama ibada mnionjeshe asali,”

alituamrisha. “Asali hatuna. Ninayo maji naye dada yangu anazo ndizi. Hakika kama mauti hatuna asali,” dada yangu alimjibu. Dada yangu, Huruma, hakujua tafsiri kamili ya ‘asali.’ “Chifu anataka tucheze mchezo wa nipe nikupe,” nilimzindua. Bado hakunielewa hadi pale nilipomweleza dhahiri shahiri kuwa chifu alitaka kutushirikisha katika mapenzi ndipo aliponielewa. Abadan katan tusingeruhusu hili kutokea. Tulikata kauli kurudi chengoni.

Njaa na uchovu zilishirikiana kama kiko na digali kutuvamia njiani. Kwa sababu ya hali hii tuliwasili nyumbani jioni hiyo. Namna iliyokuwa kawaida ya ‘mama’ zetu ndipo walipokuwa wakitoka kanisani. Ndio waliosimamia kikoa cha waimbaji kanisani mle. Baada ya vipindi vya kawaida wangesalia mle wakiwafundisha wenzao uimbaji na nyimbo mpya. Walipigwa na butwaa walipoziona shehena zilizokuwa vichwani petu. Maelezo yetu yaliyogeuka na kuwa vilio yaligonga mwamba. Yaliangukia masikio ya kufa yasiyosikia dawa wala kafara. Walishikilia kikiki wazo lao kwamba tulikataa kuuza bidhaa zao. Kila mmoja wao alifungua alichoweza kufungua. Wengine kamusi za matusi, wengine zana za vita. “Nendeni na msirudi hapa manzilini tena,” kwa kauli moja walisema. Tayari giza lilianza kuingia. Tuliwaomba waturuhusu kuondoka asubuhi. “Mtalala pale jikoni. Mapambazuko yasiwapate humo,” mmoja wao alisisitiza.

Ni katika chumba hiki nilikosa usingizi huku dada yangu akiwazia hatua bora ambayo tungechukua alfajiri kabla ya ‘wanajeshi’ kudamka. Saa tisa tulikuwa tumeondoka kuenda kusikojulikana. Baada ya safari ya saa mbili tulichoka hoi bin tiki. Tulijilaza chini ya mti tukisalimiwa na kila hali ya anga. Si manyunyu si baridi shadidi. Kufumba na kufumbua tukazinduka. Hii ilitokana na michakato ya miguu ya Faraja. Faraja alikuwa mkulima hodari aliyekuza mimea anuwai. Aliamkia shamba lake alfajiri na kurejea machweo. Hakuwa na majukumu mengi nyumbani hivyo basi angekuwa shambani mchana kutwa. Katika kipindi cha miaka hamsini pamoja na mke wake Bi. Saidia hawakujaliwa mwana. Mapato yaliyotokana na chudi zake yalioza na kuozeana benkini. Daima alijifariji kuwa akiba si mbi ingawa ya kumbi siku ya kivumbi hutia motoni. Ipo siku angepata mrithi wa mali yake. Tulimsimulia masaibu yetu. Majanga yaliyotukumba yalimshawishi kutupa hifadhi. Tulirudi naye moja kwa moja hadi nyumbani kwake.

Alitupeleka katika shule tajika kijijini mle. Kule tuliwapata walimu wenye tajriba pana katika masomo mbalimbali. Nacho kinolewacho hupata, tulifua dafu toka ngazi moja hadi nyingine. Tulisoma kwa bidi za mchwa kutoka shule ya msingi hadi ya upili. Hatimaye ghera zetu ziliza matunda matamu kama halua. Tulipata mwaliko wa kuendeleza masomo yetu ughaibuni. Huko masomo yalichukua muda mrefu sana. Miaka saba tukiwa tumezamia matopa ya vitabu. Hatukuwahi kutekwa bakunja na wasena wasio kufu yetu katika nia. Hatukuwahi kusahau kuwa nazi mbovu ni harabu ya nzima. Siku ya mahafali ilipowadia hamu ya kuwaona wazazi wetu ilitutawala. Licha ya kuwa marehemu, tulifarijika kuwa Saidia na Faraja wangechukua nafasi zao barabara. Juhudi za kuwatafuta zilishika kasi. Kokote tulikoenda hatukufua dafu. Hata kwenye ubalozi wa nchi yetu hakukuwa na uwezekano wa kuwaalika. Isitoshe taarifa za hali zao zilikuwa kaburi la baniani. Kwa miaka hii yote hakujakuwa na mawasiliano yoyote kati yetu. Siku ya siku kila mtaalamu aligubikwa na wingu la furaha jamaa zake wakimvisha vya kuvishwa. Nilimvisha dada yangu naye akanivisha. Siku ikakamilika.

Si taaluma tulizosomea, si tabia zetu katika nchi ile ya Tumaini, si bidii zetu kazini, si hamu yetu ya kudumisha uzalendo mle, zote ziliandamana kututafutia kazi katika mataifa mengi duniani.

Haukuchukua muda wa mfupa wa tembo kuoza tukapata ajira ambayo yeyote razini angetamani. Tulipata kazi nchini Urusi. Kwa uangalifu na mazingatio makubwa tulitekeleza majukumu yetu. Baada ya kuijaza mifuko yetu tulikata kauli kuwajulia hali Faraja na Saidia. “Kuna umuhimu gani kushikwa mkono na mtu usiyehusiana naye kwa damu wala kwa usaha kisha umpe kisogo? Jaza ya hisani ni hisani. Nayo ada ya mja hunena muungwana ni kitendo,” tuliukumbuka wosia wa marehemu mama yetu. Pengine alijua kuwa huenda angeiacha mikononi mwa walimwengu.

Changamoto chungu nzima zilitutinga katika safari ya kutoka nchini Urusi tulikofanyia kazi. Hii ilitokana na uhusiano mbovu wa kidiplomasia baina ya nchi hiyo na Ukreni. Mashambulizi kadha wa kadha yalishuhudiwa. Licha ya mataifa ya jumuiya ya madola kuingilia katika Urusi haikutii amri hii mwanzoni. Kutokana na vita hivi, mataifa mengi yalisitisha usafiri kutoka na kuingia Urusi. Hata baadhi ya biashara za wananchi wa Urusi zilipata pigo kubwa sana. Lengo likiwa ni kushinikiza serikali ya urusi kusitisha mashambulizi dhidi ya majirani wazalendo. Hali

hiyo ilichelewesha kusafiri kwetu kwa miezi mingine tisa. Kwa kweli kilicho na mwanzo hakikosi mwisho. Hatimaye tuliruhusiwa kuondoka ingawa hali ya taharuki ilikuwa imetwaa anga za taifa hili.

Walipoona kuwa tuliishiwa nguvu walituingoza moja kwa moja hadi nyumbani. Mzee mkongwe alikuwa amejilaza juani hajijui wala hajitambui. Anakoroma mithili ya mja aliyeitikia mwito wa usingizi wa pono. Sikuamini masikio yangu wala macho yangu nilipoambiwa kuwa ndiye aliyekuwa Bw. Faraja. Hakuweza kusema wala kuongea. Njaa ilimkodolea macho ajabu. Waelekezi wetu walitupeleka kaburini. Juu ya kaburi tulimwona mama yetu. Nilimwona Bi. Saidia akinivisha mavazi yake asubuhi ile tuliyofika kwake.

Yaliyopita si ndwele tuyagange yajayo. Dada yangu alimpeleka baba hospitalini huku mimi nikitafuta mwashi stadi ambaye angemjengea nyumba inayostahili kuitwa makao. Baba alilazwa hospitalini kwa miezi mitatu. Muda huu ulitoshwa kukamilishwa kwa ujenzi wa nyumba yake ya kifahari. Ilikuwa nyumba ambayo haikuwahi kuonekana katika taifa lile. Lilitugharimu mamilioni ya pesa. Hata hivyo hayakutoshana na gharama ya malezi aliyotupa. Shilingi milioni tano tulizotumia hospitalini pia haikulingana na gharama ya malezi aliyotupa. “Tumlipe baba nini iwe sawa na gharama ya malezi. Ni nani anayeweza kufidia malezi mema ya wazazi? Njoo uniambie ili nimfidie baba”.

Jinyakulie nakala hii ili kuzidi kusoma